As a Kenya citizen, I know that there is a law which protects me, but because they did not know that such law existed, they accepted to be violated. Right now, there is a long court process and we do not know when justice will be done. If people get to know their rights, they will be bold; they will stand firm and speak out. They will say "No; I am a Kenya citizen and I know that there is a law which protects me. I am not going to allow you to violate my rights."

Hon. Deputy Speaker, because of time---

**Hon. Deputy Speaker:** Your 20 minutes are over. Who is seconding the Motion?

**Hon. (Ms.) Lay:** Hon. Deputy Speaker, I beg to move and ask hon. Mwaura to second.

**Hon. Deputy Speaker:** Proceed, hon. Mwaura.

**Hon. Mwaura:** Ahsante, mhe. Naibu Spika. Kwanza, ningependa kumpongeza mhe. Lay kwa kuileta Bungeni Hoja ambayo tunaizungumzia kwa sababu ya kufikiria sana kuhusu lugha yetu tukufu ya Kiswahili. Nimesimama kuunga mkono Hoja hii kwa sababu ya Kipengele cha 7 cha Katiba, ambacho kinasema: -

“(1) Lugha ya taifa ya Jamhuri ni Kiswahili.

(2) Lugha rasmi za Jamhuri ni Kiswahili na Kiingereza.

(3) Serikali-

(a) itazikuza na kuzilinda lugha tofauti za wanainchi wa Kenya; na,

(b) italinda na kustawisha matumizi ya lugha za kiasili, lugha ishara ya Kenya, breli na njia nyingine za mawasiliano na teknolojia zinazoweza kufikiwa na watu wenye ulemavu.”

mhe Naibu Spika, ukiviangalia hivi vipengele katika Katiba yetu, utaona kwamba sisi kama Wakenya tumekubali kwamba lugha ya Kiswahili ndiyo lugha ya kitaifa. Hiyo ni kumaanisha kwamba lugha hii ina maana zaidi kushinda hata lugha ya Kiingereza, ambayo imetujia sisi kutokana na historia yetu – tulikuwa koloni la Uingereza. Jambo la kushangaza ni kwamba lugha ya Kiswahili bado haijatiliwa maanani kama inavyopaswa. Ndiposa namshukuru mhe Lay kwa kufikiria jinsi hii.

Tukianza hapa kwetu Bungeni, kanuni za Bunge haziko katika lugha ya Kiswahili. Kamati ya Kanuni, Itifaki na Mienendo ya Bunge inafaa kuangazia umuhimu wa kutafsiriwa kwa kanuni za Bunge kwa lugha ya Kiswahili. Mhe Lay amethibitisha kwamba unapotunga Hoja na Miswada kwa madhumuni ya kuileta Bungeni, ni lazima uandike kwa lugha ya Kiingereza. Hilo ni jambo la kufedheesha. Mimi mwenyewe nimejaribu kubuni Hoja kwa lugha ya Kiswahili lakini maafisa wa Bunge wanaopaswa kutusaidia kufanya hivyo, hawaielewi lugha ya Kiswahili. Hili ni jambo ambalo tunapaswa kuliangazia ili tuweze kuwa na wafasiri ambao wanaweza kutusaidia sisi Wabunge kujieleza rasmi katika Bunge hili.

Jambo lingine la kushangaza ni kwamba hata nakala ya Katiba ambayo nimetumia, niliponukuu Kipengee cha 7, ni nakala rasimu; siyo ile ambayo tayari imefasiriwa rasmi kama Katiba ya nchi hii. Hii ni kumaanisha kwamba tangu tulipopitisha Katiba hii mwaka wa 2010, hakuna juhudi zozote zilizofanywa na Serikali kuhakikisha kwamba Wakenya wanaweza kupata katiba hii rasmi katika lugha ya kitaifa. Ni fedheha iliyoje?

Kiswahili ni lugha ambayo ina mashiko makuu sana katika historia ya Kenya. Kiswahili ni lugha ya kiasia. Wengi watakubaliana nami kwamba Kiswahili kimetiririka kutoka kwa lugha za kiasia. Ukitembea katika nchi nyingi za kiasia utapata maneno mengi ambayo yanawiana na lugha yetu ya Kiswahili. Kwa mfano, lugha ya Kizulu kule Afrika Kusini, lugha za kizambia kule Zambia na hata humu nchini, zinawiana na Kiswahili. Mimi mwenyewe, nikiiangazia lugha yangu asilia, kuna maneno mengi sana ambayo yanawiana na Kiswahili. Sembuse kusema kwamba jina “Swahili” limetokana na jina la kiarabu ‘sawahil’ – watu ambao wanaishi katika ufuo wa bahari.

Jambo muhimu ni kwamba ukiitizama lugha hii, utaona kwamba haina watu ambao unaweza kusema haswa ndio watu ambao wanaweza kuienzi kama lugha zingine za Kikuyu, Kiluo, Kiluhya na kadhalika. Kwa hivyo, ni lugha ambayo inaweza kutujumuisha sisi kama Wakenya bila ya watu wengine kuhisi kwamba wao, kwa sababu ya lugha hii, wako sawa zaidi kuliko watu wengine. Ukiangazia changamoto ambayo sisi kama Wakenya na pengine watu ambao wametumia lugha za kigeni kama lugha zao za kitaifa, ni kwamba kunakua na kukanganya kidogo wakati dhana zako ziko katika lugha ile halafu wewe mwenyewe unajieleza katika lugha yako ya Kiswahili. Mara nyingi, watu wanakataa kuzungumza Kiswahili hususa kwa sababu za kilahaja. Hakuna shule yoyote ambako watu hufundishwa lahaja ama lafudhi. Ni muhimu Wakenya tuelewe kwamba

jinsi unavyoizungumza lugha ya Kiswahili haijalishi; hata kama umeathiriwa na lugha yako ya asili.

Mhe Naibu Spika, lahaja ya Kiswahili tunayotumia ni ya kizanzibari. Kuna lahaja nyingine za Kiswahili kama vile Kimvita, Kimtang'ata, Kipemba na kadhalika. Hata kule pwani, lugha ya Kiswahili ambayo inazungumzwa kule Mombasa ni tofauti sana na lahaja ya Kiamu, ambayo inatumika kule Lamu. Kwa hivyo, hii njia ni ya kuweza kusema kwamba watu hawawezi kujieleza kwa lugha ya Kiswahili kwa sababu katika kufundisha lugha hii kule shule, kuna mtazamo wa kuisanifisha lugha – mtazamo ambao unawafanya watu kuhisi kwamba hawawezi kuizungumzia lugha hii kwa misamiati. Kwa hivyo wanaogopa. Lakini la hashu! Ninaikataa dhana hiyo. Mara nyingi sisi, kama wanasiasa, tunapoenda mashinani tusiwe tukizungumzia wananchi wetu kwa Kiingereza. Mara nyingi tunazungumza kwa lugha ya Kiswahili. Kiwe Kiswahili sambamba ama Kiswahili kombokombo, la muhimu ni kwamba Wakenya wengi wanaweza kutuelewa vilivyo wakati tunazungumza katika lugha ya Kiswahili.

Mhe. Naibu Spika, hili ni jambo ambalo kama tunaweza kuitumia lugha hii, tunaweza kuzifungua fikra na dhana za watu wengi. Watu wengi hawawezi kuzungumza kwa lugha ya Kiingereza kwa ufasaha. Kwa hivyo, wanaogopa kujieleza kwa lugha ya Kiingereza. Wanaonekana kama ni wajinga ilhali ukiwasikiza katika lugha za mama na katika Kiswahili, wana Hoja nzuri na wanaweza kuchangia katika maendeleo, hususan ukiangazia kwamba watu wetu wengi hawajasoma vilivyo na ni wa kipato cha chini na hawajaweza kuwa na ule upana wa kujua vile mambo yanaweza kuendeshwa katika nyanja tofauti tofauti.

*(Loud consultations)*

**Hon. Deputy Speaker:** Order, hon. Members! The consultations are too high. Please, let us listen to each other.

**Hon. Mwaura:** Mhe. Naibu Spika, kwa sababu naona muda wangu umeenda sana, mara nyingi twarejelea lugha yetu ya Kiswahili kwa sababu wahenga walisema kuwa “mwenda tesi na omo marejeo ni ngamani”. Kwa sababu muda hauniruhusu na Waswahili husema “ana maneno mengi kama chiriku aliye kunywa maji ya chooni”. Mimi sijayanywa na ninaunga mkono Hoja hii.

*(Question proposed)*

**Hon. Deputy Speaker:** Hon. Members, I think we should dispose of any amendment, so that we can debate the Motion after we have passed or rejected the amendments. There was one amendment by hon. Ng'ongo. Let us dispose of the amendment first.

**Hon. Ng'ongo:** Thank you, hon. Deputy Speaker.

**Hon. Members:** Hon. Deputy Speaker, tell him to speak in Kiswahili.

**Hon. Ng'ongo:** Hon. Deputy Speaker, could you remind these Members that the Motion is in English and the amendment has to be in English? Therefore, I have to speak in English. It is not that I fear Kiswahili. If anything, Kiswahili is manufactured and made in Suba.



**Hon. Deputy Speaker:** He is quite in order within the Standing Order No.77. He has started in English and so, he can continue in English.

**Hon. Ng'ongo:** Thank you, hon. Deputy Speaker. I also rise to support this Motion. In supporting I am also proposing an amendment. I beg to move that the Motion be amended as follows:-

By inserting the words “the Constitution,” immediately after the word “translating” appearing in the fourth last sentence.

I want to congratulate hon. Lay for thinking and bringing this Motion to this House. Literacy level in this country is known. A good number of Kenyans are not able to read and understand English. Even those who are barely literate have very low command of the English Language. Kiswahili is widely spoken across the country. As a country, we want to be proud that we have a language that we speak and communicate on extensively.

If you look at the provisions of Article 10, namely, values and good governance, you realise that one of the values that are provided under Article 10, which I expect the President to address us on tomorrow, is with regard to the issue of national unity. You can only realise national unity if you have a language that unites the country. That is Kiswahili. We must congratulate and praise the former President, Daniel Arap Moi, who made Kiswahili a national language and which he gave prominence. We should also thank the education sector which made Kiswahili compulsory. That helped us when hon. Oluoch was going for a Kiswahili proficiency test before he became a Member of Parliament. I was lucky to get an exemption because I did Kiswahili in Form Four. Do not worry about whether I passed it or not, but I got some grade that was considered to be reasonable to come to this Parliament.

I have included “the Constitution.” Hon. Lay provides in this Motion that all laws made in the National Assembly and the county assemblies should be translated in Kiswahili. However, the supreme law of the Republic, namely, the Constitution, was left out in the original Motion. That is why I have recommended that we add it. If you look at Article 3 of the same Constitution, which talks about the defence of this Constitution, it says that:-

“Every person has an obligation to respect, uphold and defend this Constitution”. You can only respect, uphold and defend a document that you understand. Therefore, we need to make it possible for most Kenyans, if not all, to understand the supreme law of the land.

As I wind up, I also want to take this House through Article 35 of the Constitution, which talks about access to information. The State has a responsibility to make sure that every Kenyan has access to information. That access to information also includes this Constitution.

The final article that I want to take this House to is Article 259, which provides that:-

- “This Constitution shall be interpreted in a manner that-
- (a) promotes its purposes, values and principles,
  - (b) advances the rule of law and the human rights and the fundamental freedoms in the Bill of Rights;
  - (c) permits the development of the law; and

(d) contributes to good governance.”

This is clearly a demonstration that the Constitution is a living document. It is a Constitution that every Kenyan needs to understand. You do not have to visit legal offices and lawyers to interpret for you. It is a Constitution that all of us should be able to talk about.

When we were propagating or supporting this Constitution and campaigning across the country, I kept on telling my constituents that there was no need for them to read it because I had read and understood it for them. Yes, I am their representative, but they need to read it for themselves. I was telling them that because I know the challenge faced when a document is put in English. I would urge that people should be more innovative and start translating the Constitution and other laws, but more so, the Constitution, in our local languages. This should be in vernacular, so that my people in the village down there know exactly what the Land Chapter is all about. They should know what it says about community land, private land and land management in general. I would urge this House to pass this Motion, but with the amendment that I have just introduced.

I move the amendment and ask my friend, hon. Wario, to second the amendment.

**Hon. Wario:** Asante, Mhe. Naibu Spika. Ningependa kumshukuru Mhe. Ng’ongo kwa fursa ya kumuunga mkono kwa marekebisho ambayo ameleta katika Bunge hili. Katiba tulionayo leo ni muhimu sana kwa taifa na vizazi vinavyokuja.

Ninayo masikitiko makubwa kwa sababu Katiba ya Kenya haijatafsiriwa rasmi katika lugha ya Kiswahili; Katiba bado ni rasimu. Kipengele sabini na saba katika Kanuni za Bunge kinatambua Kiswahili kama lugha rasmi ya Kenya. Kipengele cha saba katika Katiba kinatambua kwamba Kiswahili ni lugha rasmi na tena lugha ya taifa. Iwapo Kiswahili ni lugha rasmi na tena lugha ya taifa, kwa nini Katiba hiyo haina tafsiri rasmi ya Kiswahili? Kwa sababu hiyo, mimi namshukuru mheshimiwa Mbadi kwa kuleta marekebisho haya. Nilipoongea mara ya kwanza katika Bunge hili la Kumi na Moja, hatua ya kwanza niliyochukua ilikuwa ni kupendekeza na kuandikia Kamati ya Bunge inayohusika na Kanuni za Bunge. Kwa bahati mbaya mpaka leo sijapata jawabu. Nimeomba Kamati ya Kanuni ya Bunge itafsiri Kanuni za Bunge kwa lugha ya Kiswahili. Tangu 2013 hadi leo, Kamati hiyo haijaweza kunipa jawabu kama inaweza kutafsiri Kanuni za Bunge ama la. Ninasikitika sana.

Kwa hivyo ninaunga mkono waheshimiwa Mbadi na Lay. Mimi ninaamini kwamba taifa letu litapata uhuru kamili siku ambayo mahakama itasikiza mashtaka kwa lugha ya Kiswahili na hakimu atoe hukumu kwa lugha ya Kiswahili ndiposa mshtakiwa aweze kujitetea.

Tunajigamba eti tumepata Uhuru ilhali Wachina wanatufungia hoteli hapa. Kwa nini? Ni kwa sababu tunaiga mavazi yao na lugha zao. Heshima na uhuru wetu ni mambo ambayo hayatotambulika. Kwa hayo machache, nimesimama kuunga mkono marekebisho yaliyoletwa na ndugu yangu mheshimiwa Mbadi ili Katiba itafsiriwe rasmi katika lugha ya Kiswahili. Asante Naibu Spika wa Muda.

*(Question, that the words to be  
inserted be inserted, proposed)*

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): Hon. Members, I am going to follow the list as it is here. So, please, I ask you to desist from coming to see how far your name is. I will follow the law as per the people who put in their order one after the other. I will, of course, also consider the issue of equality and gender representation.

What is your point of order?

**Hon. Letimalo:** Hon. Temporary Deputy Speaker, while you use your discretion to go by the list on the screen, I wish you can also take cognisance of the fact that some Members had logged in and they never got an opportunity to speak in the previous Motion. I urge that they be considered in the second Motion. Otherwise, Members could sit here for the whole session without getting an opportunity to contribute.

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): That is the role of the Speaker and that is what we will take cognisance of.

Hon. Members, we are now going to be contributing to this Motion as amended. I have proposed the Question already. Debate the Motion as amended. Hon. Kathuri Murungi.

*(Loud consultations)*

Hon. Members, please, do not do my work. We are debating the Motion as amended which I have proposed already. What is your point of order, hon. Mbadi?

**Hon. Ng'ongo:** Thank you, hon. Temporary Deputy Speaker. The amendment has just been seconded and the Motion is not amended yet. So, we need to either debate the amendment or dispose of it---

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): What I have read is the version that should be amended. Is that not the case?

**Hon. Ng'ongo:** Yes.

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): So, that is what we are debating.

**Hon. Ng'ongo:** First, we debate the amendment and then the Motion as amended.

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): It is exactly what I am saying but I guess it is semantics, hon. Mbadi.

**Hon. Ng'ongo:** Hon. Temporary Deputy Speaker, you cannot debate the Motion as amended because the Motion has not been amended. So, we debate the amendment first.

*(Loud consultations)*

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): Hon. Member, do you want me to read the Motion and propose it again as the amendments suggest? I am proposing and not putting the Question. I want you to debate the Motion as amended.

**Hon. Members:** Put the Question! Put the Question!

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): Hon. Members, that means that you do not want to debate the amendments. I hope you know what it means.

Thank you very much Members who have pushed for that so that we follow the procedure as it should be. So, the debate now continues. I had given the Floor to hon. Kathuri Murungi.

**Hon. Murungi:** Asante sana, Mhe. Naibu Spika wa Muda kwa kunipa nafasi hii ili nichangie Hoja hii ambayo imeletwa na Mhe. Joyce Lay.

Kwanza kabisa, naiunga mkono Hoja hii ikiwa na marekebisho ambayo yameletwa na Mhe. Mbadi. Katiba ya Kenya inasema kuwa tuko na lugha mbili za kitaifa ikiwa ni Kiswahili na Kiingereza. Sheria zote ambazo zimepitishwa Kenya hii zinafaa kutafsiriwe kwa lugha ya Kiswahili ndio kila Mkenya azielewe.

Katiba yetu inawapa Wakenya wote uhuru wa kupata habari na kujua chochote kinachoendelea. Lakini inaonekana kuwa wanaotunga sheria nchini wanawadhulumu wananchi. Ukienda kwenye korti zetu, mawakili hawapendi kuitumia lugha ya Kiswahili. Ni kama hawaelewi lugha ya Kiswahili vizuri. Kwa hivyo, wanapowatetea wafungwa, wanaitumia lugha ya Kiingereza ambayo ni ngumu. Hii inaonyesha kuwa Wakenya wanaumia na hawaongei. Hata sisi katika Bunge hili la Taifa, Seneti na bunge za kaunti, Wabunge wanafaa kupewa motisha zaidi ili waweze kuongea Kiswahili katika Bunge na kuleta Hoja kwa lugha ya Kiswahili. Nimeona Mhe. Mbadi ameshindwa kuzungumza Kiswahili akiileta Hoja yake. Ninaomba kila Mbunge ambaye analeta Hoja ama Mswada hapa, ajieleze kwa Kiswahili.

Katika Hoja hii, tunajadili vile ambavyo tutaongea kwa Kiswahili katika Bunge hili na tutaafsiri sheria kwa Kiswahili, lakini wenzangu wanaongea katika lugha ya Kiingereza. Tukae kama ndugu zetu Watanzania. Katika Bunge lao, hata yule profesa wa Kiingereza ambaye yuko pale, asilimia 90 ya wakati anaongea, anatumia lugha ya Kiswahili. Hawatumia Kiingereza katika Bunge lao. Watu wetu wote wanafaa kuelewa sheria ambazo tunatunga hapa Bungeni.

Ninaiunga mkono Hoja hii ambayo imeletwa na Mhe. Joyce Lay. Wakati tunapotunga sheria hapa Bungeni, tunaweka kwa magazeti kuwa ni lazima wananchi washirikishwe katika utunzi huu. Hata tukiweka kwa magazeti, hatuweki kwa Gazeti la *Taifa Leo* ambalo linatumika hapa nchini. Viongozi wa Bunge wanaweka ilani hizi kwa lugha ya Kiingereza kwa magazeti za *Daily Nation* na *The Standard*. Ningeomba tuanze hapa Bungeni wakati tunapowashirikisha wananchi katika kutunga sheria. Tunafaa kuweka ilani zetu na mambo ambayo tunafanya hapa Bungeni kwa lugha ya Kiswahili katika Gazeti la *Taifa Leo*. Hii itawashirikisha wananchi wote.

Ninafahamu kuwa watu wengi wamefungwa kwa makosa ambayo si yao. Watu wengi wameenda kortini na hawakuelewa vile kesi zao zinaendelezwa. Wakielezwa kuwa Katiba inawapa uhuru fulani, hawajui inapatikana kwa kipengele kipi katika Katiba yetu. Nitawaomba mawakili, kwa sababu hapa tuko na mawakili wengi, wazungumze na wengine katika chama chao cha mawakili watakapomaliza vurugu zao, wawaambie kuwa wakienda kortini, waitumie lugha ya Kiswahili ndio wananchi wetu waelewe.

Ninaona kuwa wenzangu wengi wana hamu na ghamu ya kuiunga mkono Hoja hii, ninaomba kumaliza. Ninaiunga mkono Hoja hii ambayo imeletwa na mbunge wa Taita Taveta, Mhe. Joyce Lay.

**Hon. (Ms.) Amolo:** Asante sana, Mhe. Naibu Spika wa Muda. Namuunga mkono mwenzangu Mhe. Joyce Lay kwa kuileta Hoja hii siku ya leo ili tuweze kuijadili hapa Bungeni.

Kwa kweli, litakuwa jambo la maana kabisa kama lugha ya Kiswahili itaenea kote kote katika nchi yetu ya Kenya. Tunapoingia shuleni, tunaanza kusoma Kiingereza na Kiswahili na tunaendelea vizuri. Lakini tukifika mahali fulani, hatuelewi kabisa Kiswahili kinapotelea wapi. Ukifika pale mbele katika ofisi zetu, hauoni tena Kiswahili. Tunaendelea kuongea lugha ya Kiingereza. Kwa kweli, kuna mambo mengi sana ambayo tunaweza kufanya tukitumia lugha yetu ya Kiswahili. Hasa tukiangalia zile kandarasi ambazo kina mama, vijana na wale hawajiwezi wanapewa, ziko katika lugha ya Kiingereza. Unashindwa kabisa kuwa wale ambao hawaelewi Kiingereza, watatumia lugha gani ili waweze kuzipata zile kandarasi.

Bali na zile sheria kutafsiriwa kwa Kiswahili, mambo mengi katika nchi yetu yanafaa kufanywa kwa Kiswahili. Kama mambo fulani yameelezwa ka Kiingereza, chini yake yawe yameelezwa kwa Kiswahili. Kwa mfano, kama kuna ilani ya “toilets”, pale chini kuwe na maelezo ya “vyoo”. Hii itasaidia watu kuelewa. Kama ni barabara ambayo imeelezwa ka Kiswahili, inafaa kuelezwa pia kwa Kiswahili. Kwa hivyo, tusiangalie sheria peke yake. Kama wenzangu walivyosema, kama mambo mengi ambayo yanafaa kuelezwa kwa lugha ya Kiswahili.

Jambo lingine ambalo tunataka kuangalia ni wakati ambapo tunafanya mitihani. Mitihani yetu iko kwa lugha za Kiingereza na Kiswahili. Ningeomba kamati inayohusika na elimu itilie mkazo ili Kiswahili kiwe lugha rasmi. Walimu pia wanalegea katika ufundishaji wa lugha ya Kiswahili. Utapata kuwa watoto hawapendi kuifanya lugha ya Kiswahili na wanaongea “SHENG”. Ningeomba Kiswahili kitiliwe mkazo zaidi hata katika vyuo vikuu.

Hata sisi hapa Bungeni, hatuongeti Kiswahili siku zote. Tunaongea kwa lugha ya Kiingereza. Tutawezaje kuzielewa zile sheria kama tutaendelea kuongea Kiingereza? Hata wafanyikazi tunaoretwa kutusaidia hapa Bungeni, wanapaswa kuijue lugha ya Kiswahili ili wanapotafsiri, watafsiri Kiswahili ambacho tutakielewa sisi kama Wabunge.

Jambo lingine ambalo ningetilia mkazo nikimaliza ni jambo la Bajeti. Tunapoitengeza Bajeti yetu, ni vizuri wenzetu wafahamu kuwa tunaweza kuitafsiri kwa lugha ya Kiswahili. Tusiwe tunangoja kuelezwa katika lugha ya Kiingereza. Tunafaa kuilewa Bajeti kuanzia mwanzo hadi mwisho kwa lugha ya Kiswahili.

Ninaunga mkono Hoja hii. Pia, ninamshukuru mwenzangu, Mhe. Joyce Lay. Amefanya jambo la maana sana kuileta Hoja hii ili tuijadili leo.

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): Hon. Michael Onyura of Butula! He is absent. Hon. Korei ole Lemein.

**Hon. Onyura:** I am here.

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): I was looking for you on this side. Sorry.

**Hon. Onyura:** Thank you very much, hon. Temporary Deputy Speaker. I know that we have been challenged to prosecute this Motion in Kiswahili. I can assure you that I can speak good Kiswahili. Indeed, when I address my constituents, other than the vernacular, I also use Kiswahili. However, in this particular case, I have chosen that I will use English.

I rise to support this Motion very strongly and to thank the Mover of the Motion, *Mheshimiwa* Joyce, for bringing it. I cannot say it is timely. In fact, it is overdue. The Constitution encourages and envisages public participation right up to the grassroots

level. I do not see how the public is going to participate if some of the key documents that they are supposed to be using in participation when it comes to contributions on legislation or views are in a language that the majority of people in this nation do not understand or are not competent in.

All public and official documents should, as a matter of routine, be translated into Kiswahili, given that it is a national language. How can we be saying this is our national language and yet we need Parliament or somebody to be urging those who are charged with this duty to translate documents into it? It is something that should just come routinely. Whenever there is any document, we should have English and Kiswahili versions automatically.

I want to thank those who have taken the responsibility of developing Kiswahili as a language. I know that we have many research bodies, centres and educational institutions that have taken the issue of researching and developing Kiswahili very seriously. They should continue with that job. This is normal for languages. Languages develop. Languages borrow from each other. We have many words in English that perhaps have originated from Greek, French or Hebrew. So, we should encourage such bodies to continue with the good work that they are doing to develop Kiswahili.

I am sure that the use of Kiswahili including reading documents in Kiswahili is fairly popular. I noticed this experience at the time when the draft Constitution was being discussed. I remember many sessions of civic education on the draft Constitution. It was the Interim Independent Electoral Commission (IIEC), the precursor of the current Independent Electoral and Boundaries Commission (IEBC), that had printed quite a number of documents both in Kiswahili and English. Many times whenever I carried some of them back to the village level, I found that the Kiswahili version was very popular and people would keep asking for more of them.

Further to that, if you tune into some of these radio stations, particularly all these FM radio stations, you find that the Kiswahili ones are very popular. It is just that we have taken long to realise that need. Translating our laws and the Constitution into Kiswahili will encourage people to read and be aware. As it is said: "Ignorance of the law is no defence." We must be able to create an environment and give the facilities for people to be aware and to read for themselves. This will also encourage people to get away from the saying that they do not need to read these laws because "Baba" or "Chairman", as is said, has read them. Let them read for themselves. It will make a difference even in terms of civic awareness.

If the missionaries had come and left their Bible in foreign languages or English, perhaps they would not have made the kind of impact that they made. Not only did they translate the Bible into a language like Kiswahili, but they also went further and translated it into vernacular languages. This has made a lot of difference. You go into the villages and you get an old *mama* who can extensively quote for you from her vernacular Bible verses and chapters. So, it is something that we need to encourage.

Once they have been translated, I would recommend that they are packaged in user-friendly, convenient to carry around and easy to read formats. That is also important as it encourages the readership. I know that we have had novels translated into Kiswahili. We have had classics translated into Kiswahili by prominent people like *Mwalimu* Julius Nyerere. That is the direction that we should be going.

I also support the idea that has been floated here that when it comes to signage for roads and buildings, they should be done in the two languages. They should usually be done in English and be translated into Kiswahili. You go to some of these countries like Canada where they speak both English and French and you find that many of their signage are done in both languages.

Hon. Temporary Deputy Speaker, with those comments, I support this Motion and call upon all my colleagues to support it. Thank you for the chance.

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): The Member for Narok South.

**Hon. ole Lemein:** Thank you, hon. Temporary Deputy Speaker, for giving me this opportunity to contribute to this Motion as amended. I agree with the Mover of the Motion that majority of the Kenyan people are not aware of the laws that are made in this country. There are people in this country and in this Century who are not aware of a number of articles that are in the new Constitution. I want to agree with my colleagues who said that the literacy levels in this country are low. Therefore, it calls for all the laws in this country to be translated into Kiswahili.

It beats logic when we say that Kiswahili and English are national languages---

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): Hon. Member, give me a minute. There is a point of order from hon. Aisha.

**Hon. (Ms.) Katana:** Asante sana, Naibu Spika wa Muda. Nimesimama kwa jambo la nidhamu. Kwa ajili ya umuhimu wa Hoja hii ambayo inaendelea kuzungumzwa, ningeomba tupunguze muda. Badala ya kuwa dakika kumi, ziwe angalau dakika tano ili kila mmoja aweze kuzungumza.

Asante.

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): The hon. Member for Narok South will complete his contribution and then we will put the Question.

**Hon. ole Lemein:** Thank you, hon. Temporary Deputy Speaker.

When you look at the Asian Tigers' development record and their local languages, it seems that there is a correlation between their languages and their level of development. This is because the people understand their laws and languages.

Hon. Temporary Deputy Speaker, in this country wherever there is a sign in English there should be a sign in Kiswahili that will make people understand it better. I agree that it is good for Kenyans to be innovative and creative as far as this issue of language is concerned. When it comes to agreements - in as much as my colleague has spoken about the courts of law where people might have been put behind bars for not understanding what was happening, there are so many people who have lost their property because they could not understand what the agreements said because they were written in English. Perhaps, if they were written in Kiswahili they might have gotten the concept.

Hon. Temporary Deputy Speaker, because of time and I have heard my colleague, let me stop there. I support the Motion.

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): Hon. Members, I will put the Question on the point of order raised earlier by hon. Aisha.

*(Question, that debating time be*

*reduced, put and agreed to)*

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): So, we will be speaking for five minutes each. Hon. Zainabu Chidzuga.

**Hon. (Ms.) Chidzuga:** Shukrani sana, Mhe. Naibu Spika wa Muda. Kwanza naomba kumpongeza Mheshimiwa Joyce, kwa sababu ya hii Hoja aliyoleta. Kusema ukweli, shida tuliyonayo Kenya ni kuwa sheria tukonazo nyingi lakini utekelezaji ndio shida. Ikiwa tuliweza kukipitisha Kiswahili kiwe lugha ya Taifa tangu enzi za Rais aliyestaafu Mheshimiwa Moi na mpaka leo hakijatiliwa maanani, tungependa tujiulize: Shida iko wapi? Pia tuangalie jinsi ambavyo tunaweza kuirekebisha shida hiyo ili Kiswahili kiweze kutumika hata kwenye chupa za dawa. Maelezo yawe yameandikwa kwa Kiswahili ndio yule mama kijijini asiweze kumpatia mtoto wake dawa kipimo cha zaidi.

Ninaunga mkono Hoja hii kwa sababu mengi tunayoyazungumza hapa Bungeni ni yanayomhusu mwananchi kule nyanjani. Lakini je, ni wote wanaoelewa kile ambacho tunakizungumza kwa Kizungu? Hata wakati tunapokwenda kutafuta kura zetu, sidhani kwamba tunazitafuta kwa kuzungumza Kiingereza. Tunaomba kura zetu hususan kwa kutumia lugha yetu ya taifa. Kwa hivyo, hii Hoja itaweza kutusaidia sio sisi tu kama Wabunge kuweza kueleweka kule nyanjani, bali pia wananchi ambao wanajua kukizungumza na kukisoma Kiswahili lakini hawawezi kukitafsiri Kiingereza kwa lugha ya Kiswahili.

Ukiangalia katika korti zetu, utakuta mtu amehukumiwa na hajui amehukumiwa kiviipi. Hata namna ya kuweza kuibadili ile hukumu anashindwa. Inaishia mtu huyo kutozwa pesa nyingi sana na mawakili bila kujielewa kwa sababu ataelezwa mambo ambayo si ya kweli. Lakini kwa vile anatafuta haki yake, anakubali na mwisho inaishia kuwa atafungwa licha ya kwamba ametoa pesa nyingi kwa mawakili waliomwambia kwamba wakibadilisha sehemu fulani, watapata haki yake.

Kwa hivyo, ninaunga mkono Hoja hii na nina imani na Waheshimiwa licha ya kwamba tutaweza kubadilisha mipangilio yetu ya Bunge iweze kuandikwa kwa Kiswahili, tuanzie hapo na tuweze kuona pia hata masomo katika shule zetu kama vile Jiografia na *Agriculture* zimeandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Hii ni ili tuweze kuelewa lugha hizi zote na tuweze kutumia haki zetu tukiwa tunaelewa haki zetu tunazitumia kwa njia gani.

Ningependa nikomee hapo kwa sababu naona muda hauturuhusu kuzungumza sana na kila Mheshimiwa anataka kuchangia Hoja hii. Shukrani.

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): Hon Benson Mutura.

**Hon. Kangara:** Asante sana, Mheshimiwa Naibu Spika wa Muda. Nasimama kuiunga mkono Hoja hii kama ilivyobadilishwa na kumrudishia shukrani Mheshimiwa Joyce Lay kwa kuileta Hoja hii. Ni jambo nzuri. Nataka pia kumshukuru Mheshimiwa Mwaura na Mheshimiwa Wario kwa ufasaha wao wa lugha na utamkaji mwema wa maneno usiokuwa na athari za lugha ya mama. Ninawavulia kofia.

*(Applause)*



Vile vile, nitawaomba kwa heshima na unyenyekevu wakipata nafasi, wanifunze Kiswahili pia nami niweze kukifahamu kama wanavyokifahamu. Lakini ninawatolea tahadhari, wasinifunze kupitia kwa mtandao au kwa kutumia arafa fupi maanake mimi sijaimarika kidijitali.

Kiswahili kimetiliwa mkazo sana na ni lazima tukitilie mkazo jinsi Katiba ilivyokitilia mkazo kuliko lugha nyingine zozote. Ukitazama vyuo vikuu vya Amerika, Mexico na Japan na hata nchi zinginezo duniani, wameanza kufunza Kiswahili katika vyuo vyao. Kwa hivyo, ni vyema pia sisi hapa nyumbani tukichukue Kiswahili kuwa lugha muhimu. Mara nyingi Kiswahili kimechukuliwa kama lugha ya watu hohehahe, maskini na wa chini kabisa. Sasa ni lazima tuipatie umuhimu maana ni lugha kama zile nyingine. Lazima tujivunie kama Wakenya. Hii ni lugha yetu. Kama watu wa Afrika mashariki nasi pia lazima tujivunie kwamba ni lugha yetu vile vile.

Ningeomba pia katika Bunge ni lazima tuweke mfano mzuri, tupitishe kuwa tunapopiga chapa hizi Hoja na nakala zingine ziwe zinachapishwa kwa lugha ya Kiswahili. Hatuwezi kuziambia idara zingine umuhimu wa Kiswahili ilhali sisi wenyewe hapa Bungeni hatuyafuati hayo maadili. Ninajua mawakili wengi sana wakiwa pale kortini huwa wamebobeza katika lugha za kikoloni lakini inapofika wakati wa kuzitafsiri kwa lugha ya Kiswahili huwa wanapata shida. Hapa namuona Mheshimiwa Gladys ambaye pia ni wakili lakini ninajua akiambiwa atafsiri kwa lugha ya Kiswahili atakuwa na changamoto. Kwa hivyo, katika mambo ya sheria ni vigumu zaidi. Ukiangalia mambo ya kesi inavyoripotiwa ama kuchukuliwa pale tunasema *statement*, mara nyingi inakuwa katika lugha ya Kiingereza. Hapo ndipo pana shida maanake mshatikwa mara nyingi anasomewa na kuambiwa, “hii ndio taarifa uliyosema.” Kwa vile hana ule uelewaji wa lugha inakuwa ni tatizo kwake na hata akienda kortini anakumbwa na changamoto.

Hii lugha yetu ni lazima tujivunie na tuonyeshe umuhimu wake. Mambo ya kubuni sheria na kuziandika ina shida. Katiba inatuambia Kiswahili ni muhimu. Mambo mengi katika majarida yaliyoko yameandikwa kwa Kiingereza na wakati mwingine watu hawawezi kuelewa. Naiunga mkono Hoja hii. Asante.

**Hon. Nakara:** Asante, Mheshimiwa Naibu Spika wa Muda. Nasimama kuunga mkono Hoja hii. Umuhimu wa mawasiliano ni kuwasilisha ujumbe ama habari kwa lugha inayoeleweka. Huo ndio umuhimu wa mawasiliano. Ukitaka mtu alielewe jambo, lazima utumie lugha anayoelewa. Kama tunataka Wakenya wajue sheria zetu, ni lazima tutumie lugha ambayo wanaielewa. Ingawa tunaongea mambo ya kutafsiri sheria zetu katika lugha ya Kiswahili, kuna changamoto ambazo ni lazima kwanza tukabiliane nazo ndipo lugha hii iwe ya maana kwa wananchi.

Chanagamoto ya kwanza ni kuwa zaidi ya asilimia sabini ya Wakenya hawajui kusoma. Kwa hivyo, hata ukitafsiri sheria zetu kwa lugha ya Kiswahili bado kuna shida. Jambo kuu ni kuanza kuhamasisha watu wetu waende shule. Watu wazima ambao wamepita umri wa kusoma waanze kuhudhuria madarasa ya watu wazima! Wakisha jua kusoma, hizo sheria zilizotafsiriwa katika lugha ya Kiswahili zitakuwa za umuhimu kwao.

Kama huyu hajui kusoma, hata ukitafsiri sheria hizo kwa Kiswahili, bado haina ladha wala faida kwake.

Changamoto nyingine ni kwamba maktaba ya taifa hayahifadhi Katiba katika lugha za makabila yetu. Itafika wakati ambapo watoto watakazaliwa hawatajua lugha

zao. Ni muhimu maktaba ya kitaifa ijaribu njia zote za kuhifadhi kila chombo chenye thamani. Kwa mfano, kuihifadhi Katiba katika kila lugha nchini itawasaidia wale ambao watazaliwa, baada ya sisi kuondoka, kufahamu jinsi lugha zao zilivyokuwa. Watoto wengine wanaozaliwa mijini, kama Nairobi, hawajui lugha zao. Wanajua Kiswahili na Kiingereza pekee. Inakuwa shida kuhifadhi utamaduni na lugha zetu. Tukiendelea namna hii, lugha zingine zitakuja kupotea. Siwezi kuzungumzia lugha nyingine, lakini lugha yangu ya Kiturkana itaendelea kuweko.

Changamoto nyingine ni kwamba Kiswahili simulizi ni tofauti na Kiswahili cha kuadika. Kwa mfano, Kiswahili kinachotumika katika eneo la Pwani si Kiswahili ambacho kinaweza kutumika kutafsiri sheria zetu. Kiswahili cha Pwani ni lugha simulizi. Katika lugha ya Kiswahili, kuna ngeli na herufi. Kwa hivyo, wakati tunaposema tukalimani na kutafsiri sheria zetu, ni lazima tuwe na walimu ambao wanaelewa ngeli, na wanajua kuisanifisha lugha ya Kiswahili ili mtoto atakayesoma Kiswahili aweze kutofautisha Kiswahili cha kuongea na Kiswahili cha kuandika. Kwa hivyo, kuna changamoto pia ya kuhakikisha kwamba tunafundisha Kiswahili katika shule zetu ili watoto wetu waweze kujua Kiswahili sanifu na kupata nafasi ya kuajiriwa kama wakalimani ili waweze kutafsiri sheria zetu kwa lugha tofauti.

Changamoto nyingine ni kwamba walimu wa Kiswahili katika nchi hii ni wachache. Kwa hivyo, hata tukikubaliana kutafsiri sheria zetu kwa lugha ya Kiswahili, tusipokuwa na walimu wakutosha ambao watafundisha lugha hiyo kote nchini, hatutaweza kufaulu. Kwa hivyo, tuihimize Serikali iwaajiri walimu wengi wa lugha ya Kiswahili, ili wafundishe lugha hiyo shuleni zetu, ili watoto wetu wajue kusoma Kiswahili ndiyo tuwatumie watoto hao kutafsiri sheria na vitabu vyetu kwa lugha ya Kiswahili.

Kwa hayo machache, ningependa kuiunga mkono Hoja hii.

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): Hon. Mwadeghu, please, proceed.

**Hon. Mwadeghu:** Mhe. Naibu Spika wa Muda, nashukuru kwa nafasi hii ambayo umenipatia nimpongeze mhe. (Bi.) Joyce Lay kwa Hoja hii ambayo ameileta Bungeni asubuhi ya leo. Naomba pia nitumie nafasi hii kumshukuru.

*(Some hon. Members leaned on their seats)*

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): Order! The hon. Members leaning on your seats and facing behind, please, that is not proper.

**Hon. Mwadeghu:** Mhe. Naibu Spika wa Muda, nikimkumbuka Rais wa Tanzania, mhe. Julius Kabarage Nyerere, ambaye alikitafsiri kitabu chake cha *Uhuru Wa Watumwa*, natumaini kwamba tunaelekea kupata uhuru wetu. Sheria za nchi yetu zimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Hoja hii inaomba wanaohusika watafsiri sheria zetu zote, pamoja na Katiba, kwa lugha ya Kiswahili; ambayo ndiyo lugha inayoeleweka na wengi. Tukiangalia ule udhalimu waliofanyiwa Wakenya, utaona kwamba mara nyingi waadhiriwa wanashindwa kueleza kwa lugha ya Kiingereza kwa sababu lugha ambayo wanaifahamu ni Kiswahili. Mara nyingi, washukiwa wanapopelekwa mahakamani, wakalimani ambao wameajiriwa kutafsiri lugha ya Kiingereza mara nyingi huwapotosha washtakiwa.

Mhe. Spika, tulipoipitisha Katiba mwaka wa 2010, tukaingia katika sera ya ugutuzi, moja ya vipengele ambavyo vinahusika ni makadirio ya fedha za kaunti. Makadirio hayo huandikwa kwa lugha ya Kiingereza, na watu hawaelewi. Utakuta fedha ambazo zinaombwa na kaunti zimeandikwa kwa Kiingereza na wananchi wanashindwa watajikwamua namna gani kutoka kwa hali hiyo ili wapate kuyaelewa makadirio hayo. Wakitaka kuyapitisha, mara nyingi wanayapitisha kwa sababu ya maelezo wanayopata kutoka kwa wahusika, ambao huwadanganya wananchi kua wamefanya marekebisha kwa sababu ya shida ya lugha.

Mazungumzo yetu ya kawaida hufanywa kwa Kiswahili. Ninapochangia Hoja na Miswada hapa Bungeni, mara nyingi mimi hutumia lugha ya Kiswahili. Namshukuru mhe. Lay kwa kuileta Hoja hii Bungeni, kuwashinikiza wanaohusika kuzitafsiri sheria zetu kwa lugha ya Kiswahili.

Tukubaliane kwamba vituo vingi vya redio vinavyotumia masafa marefu, ambavyo hupeperusha vipindi vyao kwa lugha ya Kiswahili, vina wafuasi wengi ambao wanavifurahia kuliko vituo ambavyo hupeperusha vipindi vyao kwa Kiingereza. Wakati umefika wa kuchapisha matangazo ya kandarasi za Serikali magazetini kwa lugha ya Kiswahili ndiyo wananchi wapate kujua ni nini kinahitajika kutoka kwao. Nikimalizia, hata Bibilia na Kuruani zimetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili. Itakuaje Katiba yetu, ambayo imebana humu nchini, ibaki kwa lugha ya kigeni pekee? Ndiyo maana Hoja hii ni muhimu sana. Ninawaomba Wabunge wenzangu waiunge mkono Hoja hii na watilie mkazo ili kila kitu chetu kipate kutafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili.

Kwa haya machache, ninaaunga mkono.

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): Yes, hon. Shaban.

**Hon. (Dr.) Shaban:** Ahsante sana, mhe. Naibu Spika wa Muda, kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuunga mkono, na haswa pia kulizungumzia suala hili ambalo dada yangu mhe. Lay ameweza kuileta hapa Bungeni – kuhusu umuhimu wa kuzitafsiri sheria zetu kwa lugha ya taifa. Ninampongeza Bi. Lay kwa kuileta Hoja hii ambayo ni ya muhimu sana.

Ukiangalia Kipengele cha 7(2) ambacho kinazungumzia masuala ya jamuhuri yetu ya Kenya, ni wazi kwamba Kiswahili ni lugha ya taifa. Kipengele cha 7(2) kinabainisha kwamba lugha rasmi za taifa letu ni mbili; Kiswahili na Kiingereza. Utaona kwamba Kiswahili kimetangulia Kiingereza kwenye mpangilio huo. Hii inamaanisha kwamba Kiswahili kina umuhimu mkubwa nchini Kenya. Kipengele cha (7) hakikuwekwa kwenye Katiba yetu kuwa pambo bali kimewekwa kwenye Katiba kuonyesha wazi umuhimu wa Kiswahili kwa nchi yetu. Kwa hivyo, kama alivyopendekeza Bi. Lay, Kiswahili kitumike rasmi kwenye sheria zetu zote. Ninapendekeza Serikali ilazimishwe kutekeleza suala hili. Suala hili halikuwekwa kwenye Kipengele cha 7 bure. Kuna umuhimu wa kuzitafsiri sheria zote za Kenya kwa lugha ya Kiswahili.

Kiswahili kimepatiwa kipa umbele kwenye jumuiya ya Afrika Mashariki pia katika Bunge la Afrika nzima ambako kinatumika rasmi. Lugha hii haikuwekwa pale kama mapambo. Inatajikana sisi tunaofahamu lugha ya Kiswahili kuwa muhimu tusukume gurudumu hili ili wengine watufuate. Lugha inatajikana iwawezeshe watu kuelewana. Lugha hutumika kuelimisha watu. Kwa hivyo tutumie Kiswahili kuwaeleza wananchi masuala yanayowahusu.

Mara nyingi, watu wengi huwa na uoga wa kuzungumza lugha hii ya Kiswahili wakifikiria kuwa kuna yule ambaye labda ana ujuzi kushinda mwingine. Nafikiria lugha huwa inazidi kukuzwa kama watu wataitumia. Ukienda Rwanda, utakuta kuwa Kiswahili kinatumika kila mahali kwa sababu pia wao wameamua kuwa Kiswahili ni lugha yao ya taifa. Kama Rwanda ambayo ni nchi ilikuwa na matatizo inatumia lugha hii, sembuse sisi Wakenya ambao tulianzisha suala hili kitambo?

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): Hon. Simba Arati, what is your point of order?

**Hon. Simba:** Hoja ya nidhamu, Naibu Spika wa Muda. Mimi nimekuja hapa kitambo sana ilhali huyu mheshimiwa ambaye yuko kwenye jukwaa---

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): She is a leader and everybody understands that.

**Hon. Simba:** Kabla hujaniambia mambo ya *leadership*, kutoka jana mpaka leo hii kadi yangu imekuwa ikiwaka na hali sijapewa nafasi ya kuongea. Nitapewa lini mimi nafasi ya kuongea ndani ya Bunge hili?

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): Please, follow the rules of the House.

**Hon. Simba:** Hilo ndilo swali ambalo nauliza. Nipe nafasi hata kama ni dakika mbili peke yake. Kwa hivyo niendeleo?

**Hon. (Dr.) Shaban:** Naibu Spika wa Muda, nafikiria bado tunahitaji mafunzo. Wengine tumekuwa Wabunge kwa muda mrefu na wengine bado tunahitaji mafunzo ili kuweza kuelewa masuala haya.

Nataka kumalizia kwa kusema kuwa mimi naunga mkono Hoja hii. Serikali iweze kuhakikisha kuwa sheria zinatafsiriwa katika lugha ya Kiswahili. Asante sana.

**Hon. Kemei:** Asante sana Naibu Spika wa Muda kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia Hoja hii. Kwanza, ningependa kumshukuru mhe. Lay kwa kuleta Hoja hii Bungeni na kuitanguliza. Vile vile, ningependa kumshukuru mhe. Mbadi kwa kuifanyia marekebisho kusudi sisi tunapoichangia iambatane na mahitaji yetu kama taifa.

Ingawa tumeitambua lugha ya Kiswahili kama lugha ya taifa na vile vile kama lugha yetu katika Afrika ya Mashariki, katika matumizi yake hatujaboresha lugha hii iwe kama lugha ya Kiingereza. Masikitiko yangu ni kwamba, hata mwenye kuileta Hoja hii Bungeni na mwenye kuifanyia marekebisho, wote wawili walitumia lugha ya Kimombo. Ningefurahi sana kama wangeitumia lugha ya Kiswahili kusudi sisi sote tuendeshe mambo yetu katika lugha ya Kiswahili ili kuimarisha lugha hiyo.

Nitaongea kwa ufupi kwa sababu kuna wenzangu ambao vile vile nao wangependa kuchangia Hoja hii. Jambo langu kuu ni kwamba Kenya na dunia nzima inapiga hatua sana katika nyanja ya sayansi, teknolojia na mawasiliano. Maendeleo hayo hayatakuwa na manufaa kwetu na kwa watu wetu ikiwa hatutatumia lugha ambayo watu wetu wanaelewa. Vile vile ningependa kituo hiki cha kunakili na kupasha habari kuhusu sheria zetu kipewe nguvu ili kufanya kazi kana kwamba mawasiliano yote ya umma, sio sheria peke yake, yaweze kutafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili kusudi watu wetu waweze kuelewa mambo ambayo yanaendelea katika nchi yetu.

Naunga mkono Hoja hii. Namsihi mhe. Lay vile vile alete mswada Bungeni kusudi tutengeneze sheria. Ahsante.

**Hon. Saney:** Thank you, hon. Temporary Deputy Speaker. Kiswahili is one of the official languages in this country---

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): Hon. Member, please, are you Ibrahim Saney of Wajir North?

**Hon. Saney:** Yes, speaking.

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): Yes, proceed.

*(Laughter)*

**Hon. Saney:** Kiswahili is one of the official languages recognized in our supreme law. What this Motion will attempt to do is to institutionalize the implementation and the use of Kiswahili as---

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): Hold on please. Hon. Dori, What is your point of order?

**Hon. Ramadhani:** Jambo la nidhamu, Naibu Spika wa Muda. Kulingana na wakati, inaonekana ya kwamba wengi wetu hatutapata fursa ya kuchambua Hoja hii. Ningeomba dakika zipunguzwe mpaka dakika tatu.

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. Ms. Shebesh): Hon. Ibrahim, finish then I will consider that.

**Hon. Saney:** The intent of this Motion is clear and is in consonance with our laws, especially the Constitution. More so, the object of this Motion is to improve the level of knowledge of the Kenyan laws. No doubt, the translation of our laws into Kiswahili will help improve the level of knowledge of our laws. However, we have to do a little bit better. We have to go beyond that to make sure that there is much beyond the translation that should enhance the knowledge of the Kenyan citizens in regard to their laws. I think that has to do with civic education so that people get these laws in many other vernacular languages. It is not only about translating our laws into Kiswahili.

We must be cognizant of the fact that many of the pastoral communities are illiterate. We have over 80 per cent illiteracy rate there. Therefore, translating our laws into Kiswahili may not achieve much. There is the perception that translating our laws into Kiswahili may improve knowledge of our laws, but the truth is that Kiswahili is much harder than English itself and that can be evidence from the fact that in terms of performance, our children perform better in English than in Kiswahili. So, it is never automatic that the translation of our laws into Kiswahili will as such enhance knowledge of our own laws. Indeed the translation of our documents into Kiswahili will at least enhance our knowledge of the laws, but one other issue, as has been alluded to by my colleague, is the fact that what is being spoken is not really an indicator of our readability of Kiswahili as a language. What is spoken is not actually real Kiswahili. Once translated, it may not assist. We may not be better than we are doing in English. I support, but it may not help our understanding in a bigger way.

With those few remarks, I support.

**Hon. Chea:** Shukrani sana, Mhe. Naibu Spika wa Muda kwa fursa hii. Naichukua fursa hii kumshukuru Mhe. Joyce Lay kwa kufikiria kuhusu swala hili.

Ninaunga mkono Hoja hii. Ningeenda kuungana na wenzangu kusema kuwa swala la lugha ya Kiswahili ni muhimu sana. Kama vile ilivyozungumzwa hapo awali,

Kipengele cha Saba cha Katiba yetu kimekiweka Kiswahili kama moja ya lugha za kitaifa. Pia, Kipengele cha 120 cha Katiba yetu kimesema kuwa baadhi ya lugha rasmi za Bunge ni Kiswahili.

Kunao umuhimu wa kuhakikisha kwamba lugha ya Kiswahili imetumiwa vyema na hasa kutafsiri Katiba yetu na sheria zetu ili kuhakikisha kwamba watu wengi wanaelewa mambo haya. Ukiangalia ndani ya Katiba yetu, kuna baadhi ya vipengele ambavyo vimesisitizwa kwamba iwapo kuna changamoto ya lugha, ni muhimu pia Serikali ihakikishe kwamba imepeana watu ambao wanaweza kutafsiri ama wakalimani hasa mahakamani.

Wakati wowote mtu anautata kuhusu lugha ambayo angependa kutumia, Kipengele cha 50 cha Katiba yetu kimesema kuwa ana haki ya kuhakikisha kwamba kuna mkalimani ambaye amelipwa ndio sheria itafsiriwe kwa ile lugha ambayo anaelewa zaidi. Umuhimu wa kuhakikisha kwamba lugha ya Kiswahili imetumika, ni jambo ambalo ni lazima tuliangalie kwa karibu.

Kwanza, mawasiliano yatakua mema kati ya wale wote ambao wanahusika katika utumizi wa maswala ya kisheria. Mengi yamezungumzwa hapa kuhusu vile mawakili na baadhi ya watu hutumia lugha hii ya Kiswahili kujiletea utajiri. Nikionekana labda natetea mawakili hawa, kati ya matawi yote ya kiserikali yakiwemo hasa mahakama, na ambayo hasa mara nyingi utata wa lugha hii hutokea, kuna umuhimu wa kuhakikisha kwamba mahakimu wetu mara kwa mara, wanapelekwa katika warsha ndio waelewe vile maswala kama haya yanaendelea.

Kwa hiyo, ningependa kusisitiza kwamba kuna haja ya kuhakikisha kuwa hata askari wetu ambao mara nyingi ndio huwa vianzilishi vya kesi hizi, wanafahamu lugha hii. Wakati wanapoandika malalamishi ya washukiwa, waiandike kwa lugha ya Kiswahili.

Ningependa pia kuungana na wenzangu.

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): What is your point of order, hon. Wanga?

**Hon. (Ms.) Nyasuna:** Hoja ya nidhamu, Mhe. Naibu Spika wa Muda. Kuna ile hoja ya nidhamu ambayo ililetwa ya kupunguza muda wa kuongea kuwa dakika tatu.

*(Laughter)*

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): I will do it after the current speaker.

**Hon. Chea:** Mhe. Naibu Spika wa Muda, kongole zangu kwa Mhe. Wanga kwa kujaribu kunena Kiswahili ambacho tunakitazamia. Ningetaka kumalizia kwa kusema kuwa katika jamii zetu, swala la watu kusoma Kiswahili limekua shida sana. Kuna watu wengi sana ambao Kiswahili hawakielewi. Kwa hivyo, ningetaka kuungana na wanenaji wenzangu ambao wamesema kuwa kuna haja ya kuhakikisha kwamba ile elimu ya watu wazima ambayo imekuwa ikitolewa imeregeshwa ndio watu waweze kurudi shule ili wapate mafunzo na wahakikishe wameelewa maswala haya.

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): Hon. Members, there was a suggestion to reduce time to three minutes. Can I hear your opinion?

*(Question, that debating time be reduced, put and agreed to)*

It will now be three minutes per Member. Hon. Ferdinand Wanyonyi.

**Hon. F. K. Wanyonyi:** Hon. Temporary Deputy Speaker, I normally speak Kiswahili when I am talking to my people at home, but I will speak in English here.

I support the Motion brought by my sister, hon. Wanjalah which seeks to translate most of our laws to Kiswahili. I want to take this opportunity to congratulate and thank His Excellency the former President Moi, for having made Kiswahili a national language. We should be proud of it because of the way the people of Mombasa speak Kiswahili. I urge the Government to give more money to the National Council for Law Reporting to be able to translate most of these laws into Kiswahili. At the moment, Bibles and Qurans have been written in Kiswahili. Kiswahili is taught and examined in schools. It is mandatory these days. Before you get a job, they ask you whether you passed in English or Kiswahili. There is no need for us to waste time on this.

Secondly and more importantly, is the fact that if we leave things as they are, we run a danger of distorting the original Kiswahili and instead coming up with “SHENG.” The youth are now using “SHENG.” which you may not understand. If we leave it as it is, we will have a language problem. Therefore, it is necessary for us to allocate enough money. I want to ask the Budget and Appropriations Committee to do this in the Supplementary Budget, so that we can give money to the Council and have some of these laws translated into Kiswahili.

About 90 per cent of Kenyans can read and write. In most cases, prescriptions are written in English. Many people do not understand those prescriptions particularly our mothers and those who are half literate. Therefore, this forces the pharmacists to put most of this literature in Kiswahili for our people to be able to understand the prescriptions.

With those few remarks, I support.

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): Hon. Kamoti Mwamkale.

**Hon. Mwamkale:** Asante sana, Mhe. Naibu Spika wa Muda kwa nafasi hii. Kwanza, ninampongeza Mhe. Lay kwa kuleta Hoja hii ambayo wakati wake umefika. Imesemwa hapa kwamba Kifungo cha Saba cha Katiba yetu kii wazi ya kwamba lugha ya Kiswahili sio lugha ya kitaifa tu, bali ni lugha rasmi ya nchi hii. Kifungu hicho kinaendelea kusema kwamba Serikali ina jukumu la kuhakikisha kwamba Kifungu hiki kinatekelezwa. Hivyo basi, ninapendekeza ya kwamba, hata baada ya hoja hii kupita, Bunge hili lije na sheria ya kuisurutisha Serikali itekeleze haya yote.

Nitamalizia kusema kwamba katika sheria zetu za jinai kama *Penal Code na Criminal Procedure Code*, kuna msemo wa Kizungu ambao unasema kuwa “*ignorance of the law is no defence in court*”. Mtu hawezi kusema hakujiua wakati ameshtakiwa na kosa ambalo amelitenda.

Ukweli wa mambo ni kwamba magereza yetu yamejaa watu ambao wamehukumiwa kwa makosa ambayo hawakuyaelewa kwa sababu hawaelewi sheria zinasemaje wala hawajui wanatakikana wafuate utaratibu gani. Huwezi kumwambia mtu afuate sheria wakati sheria unayomwambia afuate haijui. Kwa hivyo kuna haja

tuhakikishe kwamba sheria hizi ziko katika lugha inayojulikana na wengi. Natambua ya kwamba kati ya lugha zote, lugha ya Kiswahili inajulikana na wengi, sio katika eneo la Pwani peke yake bali mpaka Nyanza na Mandera. Wengi wanaelewa lugha hii. Hata wale ambao hawakupata elimu ya kawaida wameenda ngumbaru na wanazungumza Kiswahili. Kama vitabu vyetu vya sheria na sheria tunazozitunga hapa zitakuwa katika lugha ya Kiswahili, nina imani kwamba Wakenya wengi watafuata sheria na megereza yetu hayatakuwa na watu ambao hawana hatia lakini wako huko kwa sababu ya ukosefu wa kuelewa sheria ambayo wanatakikana waifuata.

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): Hon. ole Ntutu!

**Hon. ole Ntutu:** Asante sana, mhe. Naibu Spika wa Muda kwa nafasi hii uliyonipa. Nampogeza mhe. (Bi.) Lay kwa kuleta mjadala huu. Mjadala huu ni muhimu sana kwa sababu asilimia kubwa ya wananchi wa Kenya hawajasoma na hawaelewi lugha ya Kiingereza. Kama tulivyosikia kutoka kwa mhe. (Bi.) Lay, wale ambao wanastahili kutafsiri Katiba na sheria nyingine hawana fedha. Ni jukumu letu kama Wabunge kuhakikisha kwamba wana fedha ili waweze kufanya kazi hii. Juzi nilikuwa nikifuatilia mjadala wa Bunge la nchi jirani ya Tanzania. Kwa kweli, nilifurahishwa sana na jinsi Wabunge walivyokuwa wakiendesha mjadala wao. Mjadala ambao ulikuwa unaendelea ulikuwa muhimu sana kwa sababu Wabunge walikuwa wanachangia wakijua wanachozungumzia. Najua wenzangu wengi hapa hawapendi kuzungumza kwa lugha yetu ya taifa. Wakati umefika kwa sisi pia hapa Bungeni kujifunza kuzungumza kwa lugha yetu ya Kiswahili. Ukienda katika nchi za ng'ambo, kama Uholanzi, utaona kwamba ijapokuwa Kiingereza kinatumiwa, wanahakikisha kwamba wanatumia lugha ambayo inajulikana na watu wengi. Ukiangalia shuleni, kortini au hata katika kuandika kandarasi, utaona kwamba lugha inayotumiwa ni ile ambayo wengi hawajui. Ndiposa nataka niseme kwamba---

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): Hon. Njuki!

**Hon. Njuki:** Thank you, hon. Temporary Deputy Speaker, for giving me the opportunity to contribute to this Motion. I have been here since morning.

Kiswahili is one of the national languages in Kenya. It is compulsory in schools. It is very close to our hearts and definitely most people speak it. Approximately 90 per cent of Kenyans speak and understand Kiswahili; even those who cannot write it. Every court in Kenya today has an interpreter because the judges and the magistrates normally speak in English. The interpreters are usually there to interpret to the people who are involved, either in Kiswahili or vernacular. Definitely, if this is used in court and it is embedded in the law being used in court, we will not need these interpreters and definitely we are going to save money for this country and make it even more efficient.

There will be challenges because there are terminologies in the English format of the Constitution that cannot have a very direct translation and retain the meaning. Definitely, we will lose a bit of the meaning. In other instances, we will have to merge languages and we will have to allow "SHENG" inside there. We cannot have law taught in English and then implemented in Kiswahili. We will have to insist that the law schools use Kiswahili as a language of communication and a form of schooling so that we do not have challenges in interpreting the law when it comes to implementation.

Lastly, if you look at the Elections Act, we have put the level of education so low that some of the lawmakers we have in county assemblies cannot communicate in



English. Therefore, it is going to be beneficial to them so that we can have involvement of everybody in the community.

With those few remarks, I support.

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): Hon. (Ms.) Nyasuna!

**Hon. (Ms.) Nyasuna:** Asante sana mhe. Naibu Spika wa Muda kwa kunipatia fursa hii. Moyo wangu ulikuwa unadundadunda kwa sababu nilikuwa nimetafuta Kiswahili chote na nilikuwa naona muda unaisha kabla sijatumia Kiswahili hicho.

Ninatoa shukrani kwa mhe. (Bi.) Lay kwa kuileta Hoja hii ambayo inatupatia nafasi ya kuzungumza kwa Kiswahili. Wabunge ambao wanatuongoza katika lugha hii ni mhe. (Bi.) Khamisi na mhe (Dkt) Shaban lakini leo mhe (Bi.) Lay ametuweka katika nafasi ya sisi pia kutumia Kiswahili. Nataka iende katika kumbukumbu za Bunge hili kwamba mimi nilipata alama 'A' katika somo la Kiswahili katika mtihani wa kidato cha nne (KCSE). Kiswahili cha kuandika nakijua lakini kile cha kuongea ni tofauti.

Mhe. Naibu Spika wa Muda, ukiwa kwa kiti leo, tunakupatia changamoto hata wewe pia uongee kwa Kiswahili ukituongoza katika majadala huu kwa sababu kama mimi naongea, sembuse mhe. Naibu Spika wa Muda!

Mjadala huu ni wa kikatiba. Ukiangalia Kipengele cha (35), utaona kwamba kila mwananchi ana haki ya kupata habari kutoka kwa ofisi ya umma na habari zozote ambazo mtu mwingine anazo ambazo zinahitajika ili kutekeleza au kulinda haki yoyote au uhuru wowote wa kimsingi. Katiba inasema kwamba kila mtu ana haki ya kupata habari. Habari hiyo ikiletwa kwako katika lugha ambayo huielewi, basi hujapata habari hiyo na hivyo basi Katiba itakuwa imekeuka. Kile ambacho kinatatanisha ni huu mtazamo kwamba Kiswahili ni lugha ya watu wenye tabaka ya chini ilhali Kiingereza ni lugha ya watu wenye tabaka ya juu. Hapa Nairobi, utaona watu wa Eastlands wakizungumza kwa Kiswahili na watu wa Kileleshwa, Lavington na Runda wakizungumza kwa Kiingereza. Ule mtazamo wa kukiweka Kiswahili kama lugha ya watu wenye tabaka ya chini si mzuri kwa sababu hii ni lugha ya kitaifa.

Mhe. Naibu Spika wa Muda, ukiingia ndege ya Kenya Airways huko Uchina halafu usikie wanasema "karibu sana katika ndege hii yetu ya Kenya Airways", unasikia uko na fahari.

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): Asante sana Mheshimiwa Wanga. Ulikuwa na hamu ya kunisikia nikiongea Kiswahili. Kiswahili changu ni hicho cha Nairobi ambacho umesema ni cha taratibu.

Mheshimiwa Paul Koinange.

**Hon. Koinange:** Thank you, hon. Temporary Deputy Speaker. I would like to support this Motion by hon. Joyce Wanjalah. We have very many language experts who can be able to make this effort of self-liberation possible in Kenya today. Every year we train, examine and also graduate translators and interpreters in our Kenyan universities. Ours is just to give direction to the members of this nation on how we can go on about translating our laws into Kiswahili.

To be specific, on 23<sup>rd</sup> April, 1931 a delegation from Kenya led by James Mutua of Akambaland---

*(Hon. Koinange spoke off the record)*

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): Please, press the intervention button.

**Hon. Koinange:** Thank you, hon. Temporary Deputy Speaker. I was saying that a delegation went to England to meet the Queen. To be specific, on 23<sup>rd</sup> April, 1931 this delegation from Kenya comprised of James Mutua from Akambaland and Ezekiel Apindi of Kavirondo Taxpayers' Welfare Association. They sent the same sentiments that we are discussing in this House today.

Hon. Temporary Deputy Speaker, I am convinced that if we change and translate our laws into Kiswahili then many laws that are broken by our people will not be broken. In those years of 1930s, the British Government was very concerned because they were not able to rule because of the laws which were suppressing and Kenyans did not understand them. Similarly, in 2010, if the laws were already interpreted we would not have gone through what we did during the changing of our Constitution. We went through a very expensive exercise and at the same time, many people were left very bitter.

I want to support and recommend that we pass a regulation where we will require that all Bills are translated into Kiswahili. So, in the near future and according to Article 7(1) and (2) of the Constitution, we will not be breaking the law.

Thank you, hon. Temporary Deputy Speaker.

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): Mheshimiwa George Theuri.

**Hon. Theuri:** Asante sana, Mheshimiwa Naibu Spika wa Muda. Nasimama kuchangia Hoja hii.

*(Applause)*

Kiswahili ni lugha ya taifa na ni muhimu tuelewe kwamba sio Wakenya wote wanaofahamu Kizungu. Kusudi sote tuweze kuwa na usawa, ni muhimu sheria ya nchi ichapishwe kwa lugha ya taifa. Tuna watu wengi ambao wangependa kujua na kujisomea sheria. Ili tuwezeshe hawa Wakenya wenzetu kufaidika, ni lazima tuchapishe sheria kwa lugha iwezayo kueleweka kwa urahisi ambayo ni lugha ya taifa. Ili tuweze kujivunia uhuru wetu, ni muhimu tuchapishe sheria kwa lugha ya Kiswahili tunayojivunia. Ni lazima tujikomboa na tuchapishe sheria kwa lugha ya taifa.

Naunga Hoja hii mkono. Asante sana.

*(Applause)*

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): Mheshimiwa Joseph wa Igembe Kaskazini.

**Hon. M'uthari:** Asante Naibu Spika wa Muda. I rise to also support this Motion and I thank---

**Hon. Members:** Tumia Kiswahili.

**Hon. M'uthari:** No. I have freedom to use the language I would like to use. So, I rise to support this Motion.

**Hon. (Ms.) Nyasuna:** Jambo la nidhamu, Naibu Spika wa Muda.

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): There is a point of order. Today you have very many---

**Hon. (Ms.) Nyasuna:** Asante sana Mheshimiwa Naibu Spika wa Muda. Sheria za Bunge zinasema kwamba ukianza na lugha moja utaendelea nayo. Mheshimiwa M'ruaki alianza kwa Kiswahili. Kwa hivyo, aendelee nacho.

*(Applause)*

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): Ni ukweli. Endelea kwa Kiswahili tafadhali.

*(Laughter)*

**Hon. M'uthari:** Okay. Asante, Mheshimiwa Naibu Spika wa Muda. Mimi pia nimesimama kuunga mkono Hoja hii. Hii Hoja ni muhimu sana kwa sababu tunajua lugha ya Kiswahili ni lugha ya kitaifa na inayoeleweka sana katika nchi yetu ya Kenya. Kwa hivyo, tukitafsiri Katiba yetu iwe kwa lugha ya Kiswahili, itakuwa ya manufaa kwa sababu watu wengi Kenya wataweza kuelewa.

Pia tunajua umuhimu wa lugha. Lugha ndiyo njia ya kueneza utamaduni wa watu. Nchi nyingi kama Uchina na Ulaya wanatumia lugha zao. Pia tunasambaza utamaduni wa Waingereza kwa kutumia lugha yao. Ukiona Waitaliano na Wafaransa, wao pia wanatumia lugha zao. Kwa sababu Kiswahili kimekuwa sio lugha ya Kenya pekee bali lugha inayotumika eneo la Afrika naamini kuwa hata nchi nyingi za Afrika kama eneo la Jumuiya ya Afrika Mashariki utaona kuwa nchi nyingi zinatumia lugha ya Kiswahili. Tunaangalia hata zile nchi za Afrika ya Kati wanapotumia Kiswahili. Tunahitaji tuwe hata na pesa iliyowekwa kueneza lugha ya Kiswahili tutakapokutumia kwa Katiba kwa sababu njia hiyo itasaidia kukuza utamaduni wetu na sisi watu wa Kenya. Ukiangalia utaona kuwa watu wengi Kenya hawaelewi hata majukumu tofauti yaliyopeanwa na hii Katiba yetu ya 2010. Ukiangalia kazi za zile serikali za mashinani na Serikali Kuu utaona kuwa watu hawaelewi.

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): Mheshimiwa. Mishi Juma.

**Hon. (Ms.) Khamisi:** Asante sana, Mheshimiwa Naibu Spika wa Muda. Nasimama kuunga mkono Hoja hii iliyoletwa ni dadangu Mheshimiwa Joyce Lay. Kwanza nataka kusema ikiwa Kiswahili ni lugha rasmi na ya kitaifa ni lazima tuitukuze na kuienzi kwa mahaba kama tunavyoipenda lugha ya Kiingereza ambayo tuliletewa na wakoloni.

Nataka kusema kuwa Katiba yetu ya sasa ni sheria mama na ndiyo inasimamia utawala wa nchi yetu. Vipi Katiba hii itakuwa haijatafsiriwa kwa Kiswahili? Hili ni suala ambalo lazima sisi watungasheria katika Bunge hili tunafaa tuliangalie kwa undani sana. Katika utekelezaji wa sheria, lazima washikadau husika wahusishwe katika mambo ya sheria.

Kwa mfano, mshikadau ambaye ni mahakama; ambayo inatoa hukumu kwa wale ambao wamekiuka sheria, ni lazima aelee sheria hii. Wenye kutunga sheria, kama sisi Wabunge katika Bunge hili, ni lazima tuzielewe sheria ili tuweze kufanya utekelezaji. Pia

Wakenya ni lazima wazielewe sheria hizo kinaga ubaga ili waweze kuzifuata na kuepuka kufanya maovu, kinyume na sheria hizo.

Mhe. Naibu Spika wa Muda, katika barabara zetu hapa Kenya tunaona kwamba kuna sheria ambazo zimewekwa. Kwenye kibao, utaona kumeandikwa “Keep Left” kwa Kiingereza ama “Keep Right”. Kwa Mkenya ambaye hajui lugha ya Kiingereza, huoni kwamba anaweza kufanya ajali kwa sababu ya kutojua lugha iliyotumiwa kwenye alama ile? Akina mama wengi na mabanti wetu wadogo, ambao wanabakwa, wanaelewa Kiswahili. Wanapokwenda kwenye afisi za wahusika wa kisheria kuandikisha taarifa kuhusu dhuluma ambayo wamefanyiwa, wengi wao hawawezi kuandikisha taarifa kwa Kiingereza. Hivyo basi, mhasiriwa anapoandikisha taarifa yake kwa Kiswahili, afisa wa polisi anamwambia: “Dada, ninaweza kukutafsiria taarifa hii kwa lugha ya Kiingereza.” Je, banati huyu, ambaye ni mchanga wa umri, na ambaye hafahamu sheria zetu, atawezaje kujua kwamba taarifa yake imeandikwa kwa lugha inayofaa na kwa yale malengo yanayohusu dhulma aliyofanyiwa? Hata katika jela zetu---

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shabesh): Yes, hon. Wafula Wamunyinyi.

**Hon. Wamunyinyi:** Ahsante, mhe. Naibu Spika wa Muda, kwa kunipa fursa hii ya kuichangia Hoja hii.

Kwanza, ningependa kumpongeza mhe. Lay kwa kuileta Hoja hii yenye umuhimu mkubwa katika nchi yetu. Mbali na umuhimu wote na sababu zilizotolewa za kuitafsiri Katiba, pia lugha ya Kiswahili kama lugha tunayoongea sisi tukihutubia watu wetu kule mashinani, ndiyo lugha ambayo inafikia wananchi wengi zaidi kushinda lugha nyingine zozote nchini Kenya. Kiswahili ni lugha ambayo unaweza kuiongea mahali popote nchini Kenya na ueleweke. Pia, ndiyo lugha ambayo itatuwezesha kuwaunganisha Wakenya. Ni lazima Wabunge wenzangu pia wajue kwamba Umoja wa Afrika unakitambua Kiswahili kama lugha rasmi katika bara la Afrika. Unaweza kuzungumza Kiswahili kwenye mkutano rasmi mahali popote barani Afrika. Katika Jumuiya ya Afrika Mashiriki, nchi kama Rwanda na Burundi, ambazo zilijiunga na jumuiya hivi karibuni, lugha yao rasmi ni Kifaransa, lakini nchi hizo zinageuza lugha yao rasmi. Hivi sasa, Rwanda na Burundi zinatambua Kiswahili. Uganda pia wamebadilisha mfumo wa elimu na sasa wanafunza Kiswahili shuleni.

Kwa hivyo, inafaa tuhakikishe kwamba tumeipitisha Hoja hii ili iweze kutekelezwa haraka ndiyo Katiba yetu itafsiriwe ili wananchi wa Kenya waweze kuisoma na kuielewa ndiyo waweze kupata haki zao. Wakenya wengi hawajui yale yaliomo ndani ya Katiba. Nimefurahi leo kumuona mhe. Nyasuna akivisoma Vipengele vya Katiba ambavyo vimempatia mwananchi haki zake. Iwapo mwananchi anaweza kuisoma Katiba ya Kenya na kuielewa, ataweza kudai haki zake ama kuhakikisha kwamba haki zake zinalindwa. Kwa hivyo, ninaiunga mkono Hoja hii na kumpongeza tena mhe. Lay. Nawaomba Wabunge wenzangu waiunge mkono Hoja hii, tuipitishe ili iendelezwe na kuwa Mswada ndiyo tuipitishe na kuwa sheria.

Kwa hayo machache, ninaunga mkono.

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shabesh): Yes, hon. Ramadhani.

**Hon. Ramadhani:** Ahsante, mhe. Naibu Spika wa Muda. Moja kwa moja, ninaiunga mkono Hoja hii, ambayo imeletwa na mhe. Lay. Kabla sijaendelea, ningependa kumpa Mbunge wa Kisauni, mhe. Bedzimba, dakika moja na nusu ya. Mhe. Naibu

Spika wa Muda, Wakenya wengi wanaitambua lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo, ni muhimu, kama viongozi, kutambua umuhimu wa Hoja hii. Mfano nzuri ambao nitauzungumzia leo ni tofauti zinazoibuka wakati tunapoleta Bungeni Miswada iliyobuniwa kwa Kiswahili na ile iliyobuniwa kwa Kiingereza. Kwa hakika, kule mashinani, wananchi hutiririka kwa wingi kutazama runinga mjadala unapofanywa kwa Kiswahili. Kwa hivyo, ninawaomba viongozi wenzangu; tuipe kipa umbele Hoja ili tuhakikishe kwamba Kiswahili kimeimarishwa humu nchini.

Kwa hayo machache, ninaiunga mkono Hoja hii na kumpa fursa mhe. Bedzimba.

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): Mhe. Ramadhani, huwezi kupeana fursa yako kwa mtu mwingine. Tafadhali, tumia dakika zako zote ama upoteze muda uliosalia.

**Hon. Ramadhani:** Ahsante, mhe. Naibu Spika wa Muda.

Kiswahili ni lugha ambayo ina umuhimu kwetu sisi Wakenya. Ni lugha ambayo inatuelekeza katika shughuli zetu za kila siku. Kwa hakika, idadi kubwa ya Wakenya hutumia Kiswahili katika kila jambo wanalolifanya kwa sababu hiyo ndiyo lugha ambayo inafahamika vyema. Kwa hivyo, tunapotunga sheria na kufanya jambo lolote, ni lazima tufahamu kwamba wakenya ndio muhimu. Tunafaa kuhakikisha kwamba jambo hili limefahamika.

Kwa hivyo, ninaiunga mkono Hoja hii.

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shabesh): Yes, hon. Gikaria.

**Hon. Gikaria:** Ahsante, mhe. Naibu Spika wa Muda, kwa kunipatia fursa hii niichangie Hoja hii. Ninaiunga mkono Hoja hii ambayo imeletwa na dada yetu. Mimi ni mwanachama wa Kamati ya Utekelezaji wa Katiba.

**Hon. Bedzimba:** Hoja ya nidhamu, mhe. Naibu Spika wa Muda.

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): Kuna nini, mhe. Rashid Juma?

**Hon. Bedzimba:** Ahsante, mhe. Naibu Spika wa Muda. Nimesimama kwa Hoja ya nidhamu, nikijua kwamba una uwezo wa kuamua ni nani anafaa kuongea. Ninaona kwamba kuna upendeleo humu ndani. Nimekuja Bungeni mbele ya mhe. Ramadhani lakini amepewa nafasi nami bado sijaongea. Kwa hivyo, ninaomba kwamba iwapo kuna Waheshimiwa wengine ambao hawaruhusiwi kuzungumza tuambiwe tujue ndiyo tukae mpaka muda uishe twende zetu. Ninaomba majina ya wanaongojea kuzungumzwa yawekwe mahali ambapo tutayaona ndiyo kila mtu ajue ni nani anafuata mwingine.

Ahsante.

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): Go on, *mheshimiwa* Gikaria.

**Hon. Gikaria:** Ahsante, Bi. Naibu Spika wa Muda.

Ninaiunga mkono Hoja hii. Niko kwenye Kamati ya Utekelezaji wa Katiba, ambayo inaangalia mambo yote yanayopitishwa Bungeni ili kuhakikisha kwamba yametekelezwa. Kwanza, Hoja hii haihitaji senti ndiyo Mkuu wa Sheria aweze kuitekeleze, isipokuwa senti kidogo tu ambazo zitatumika kwa uchapishaji wa sheria. Nilipata nafasi siku moja kuwa katika gereza. Ni kweli kwamba wafungwa wengi wanaumia sana kwa sababu ya kutoelewa sheria ambayo imeandikwa kwa lugha ya Kizungu. Kwa hivyo, kama alivyosema dada yetu, sheria zetu zikitafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili, utakuwa msada mkubwa sana kwa wale wote ambao wako magerezani. Wale

amabo watapelekwa kortini, wataweza kutumia sheria ambazo tuko nazo kujitetea. Ni kweli kwamba nchi hii haijafikia kiwango cha kuwa na mawakili ambao wataweza kusaidia watu wanyonge. Kwa hivyo, masuala mengi ya kisheria yawekwe kwa Kiswahili.

Hata hivyo, Kiswahili si lugha rahisi. Ni lugha ambayo ni lazima kila mtu aisome ili aweze kuilewa kwa undani. Mambo mengi ambayo yanaweza kutafsiriwa kutoka Kiingereza hadi Kiswahili, utapata hata Kiswahili ni kigumu zaidi kuliko Kiingereza. Hata hivyo, ningetaka kumshukuru dada yangu kwa kuileta Hoja hii na tutaitekeleza zile siku 60 sitakapomalizika.

**Mhe. (Ms.) T.G. Ali:** Asante, Mhe. Naibu Spika wa Muda. Nasimama kuichangia Hoja hii. Ningependa kumshukuru dada yangu Mhe. Lay kwa kuileta Hoja hii Bungeni. Ni haki ya Wakenya kupata Katiba iliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Hili si ombi wala ni lazima. Ningependa kuwakosoa walioandika Katiba ya Kenya na kukosa kuiandika kwa lugha ya Kiswahili. Hii ni haki ya Wakenya wote.

Watu wasipoelewa Katiba, ni vigumu sana kwao kujitetea popote Kenya. Hoja hii ni muhimu. Ningependa kuwahimiza wale ambao wanahusika, wahakikishe kwamba Katiba ya Kenya ambayo ni sheria kuu ya kuwasaidia wananchi wote wa Kenya, imetafsiriwa kwa Kiswahili ndio Wakenya waelewe vizuri jinsi ya kujitetea. Kwa hivyo, Hoja hii imeletwa wakati unaofaa. Ingeletwa hapo mbeleni lakini ningeomba tuitipishe ndio tuhakikishe kwamba Wakenya wanafaidika.

**The Temporary Deputy Speaker (Hon.) (Ms.) Shebesh:** Mhe. (Ms.) Katana.

**Mhe. (Ms.) Katana:** Asante, Mhe. Naibu Spika wa Muda. Nataka kuichukua nafasi hii kwanza nimpongeze Mhe. Lay kwa kuileta Hoja ambayo ni muhimu sana katika taifa letu la Kenya na katika Bunge hili kwa jumla.

Wakenya waliandika historia tarehe 27/8/2010 kwa kupitisha Katiba ambayo ni mwongozo katika taifa hili letu la Kenya. Lakini, Wakenya wengi kuhakikisha kwamba Katiba inawalinda, lazima waifahamu. Lugha ambayo inafahamika kwa urahisi na wananchi wengi katika taifa hili ni lugha ya Kiswahili. Hakuna mtu ambaye anaweza kujivunia Kiswahili na kusema ni lugha yake. Ni lugha ambayo imetumika katika taifa hili na 1974, ilitangazwa rasmi kuwa lugha ya kifaifa. Inatumiwa na makabila mbalimbali katika taifa hili. Kiswahili kinaleta jamii za Wakenya pamoja. Hivyo basi, ni vyema sheria na stakabadhi zote muhimu katika taifa hili zitafsiriwa katika lugha inayoeleweka na wengi.

Katika ununuzi wa zabuni, ambao hata Rais wetu wa Jamhuri ya Kenya amesisitiza sana kwamba asilimia 30 zienda kwa kina mama na vijana, ukiangalia sheria za ununuzi wa zabuni katika taifa hili, zimeandikwa kwa lugha ambayo kina mama na vijana katika Jamhuri yetu ya Kenya hawazielewi. Hivyo basi, wale mabwenyenye waliobobea katika fani hizo na wenye kuelewa lugha ya kimombo wanajivunia na kufaidi katika taifa hili na kuwacha wengine wakiwa katika hali za upweke.

Mataifa mengi ambayo yameendelea katika dunia ni yale ambayo yameandika sheria zao katika lugha ambazo zinazungumzwa kwa wingi katika mataifa yao. Nasisitiza na kuunga mkono ya kwamba sheria na Katiba katika Jamhuri yetu ya Kenya iandikwe na kutafsiriwa kwa Kiswahili.

**The Temporary Deputy Speaker (Hon.) (Ms.) Shebesh:** Muda wako umeisha. Mhe. Ekomwa.

**Hon. Ekomwa:** Hon. Temporary Deputy Speaker, because the Motion is in English and the Mover moved it in English, it is in order for me to contribute in English. When the law will be passed, I will abide by it.

It is very true that Kiswahili is a national language and we have to put it in action. When the Constitution stipulates very clearly that Kiswahili is a national language, we have to implement it in every Ministry, sector, section and office in Kenya. We must actually put it in action. It is not in order for us to have a Constitution that says something and we do not implement it. If we do not translate our Constitution into Kiswahili, it means that we are still colonized. The English that we use is a language that was brought by the colonialists. As we continue using this language, it means we are colonising ourselves.

Hon. Temporary Deputy Speaker, as you sit there and even the other Members who are seated here, are you thinking in English, Kiswahili or your mother tongue? The truth of the matter is that our intelligence is consistent to our own mother tongue or the language that you understand. For us to promote intelligence in this nation, we need to use a language that is consistent to our intelligence.

I support this Motion that we need to respect our language. By using this language, we will be promoting and boosting the East African unity. In Uganda and Tanzania, they are using Kiswahili. What is so special for us not to use Kiswahili? We claim to be Kenyans. When people vote, they vote in Kiswahili. That is one thing I am sure of. About 90 per cent of Kenyans understand Kiswahili. I have studied Epistemology, which is the study of sources of knowledge. For you to have knowledge, you must use the language that is so consistent and one that you understand. For us to enjoy the rights in this Constitution, we must use a language that is being used by many Kenyans.

I support this Motion.

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): Hon. James Kimaru. He is absent. Hon. Rashid Juma.

**Hon. Bedzimba:** Asante sana, Mhe. Naibu Spika wa Muda. Nashukuru kupata fursa hii. Waswahili wanasema “chelewa ufike”. Nimefika sasa. Lugha ya Kiswahili si lugha tu ya taifa, ni lugha rasmi ya taifa la Kenya. Kiswahili kimeangaziwa sana kama ni lugha ya watu maskini ingawa si kweli bali ni unyanyasaji kwa wale wanaotumia Kiswahili. Kutafsiri sheria za Kenya kwa lugha ya Kiswahili kutawawezesha wengi kuelewa ikiwa waliosoma na hata ambao hawakusoma. Ile lugha inayotumika ya Kiingereza ni ya ndani sana ambayo si rahisi mtu kuielewa. Kwa hivyo, ni vyema sana sheria hii itafsiriwe kwa Kiswahili.

Viongozi wote ambao wako hapa, karibu asilimia 90, wameletwa hapa kwa sababu ya lugha ya Kiswahili. Si rahisi kuwapata viongozi ambao wanatoa ahadi wakati wanaomba kura kwa lugha ya Kiingereza. Wengi wanazungumza Kiswahili lakini wanapokuja hapa kidogo wanaona kwamba lugha ya Kiswahili ni ya chini. Hii si kweli. Mataifa mengi ambayo yanatumia lugha zao yameendelea mbele sana. Ukiangalia Bara la Waarabu, Uchina na Hispania, wanatumia lugha zao ndio sababu wameendelea mbele haraka. Hata nchi jirani ya Tanzania, uchumi wake unakua kwa kasi sana kwa sababu ya kutumia lugha yao. Sisi tunatumia lugha ya wakoloni waliotufunga. Tumeikuza lugha yao na yetu tukaipuuza. Ndio sababu hawachukui nafasi kujifundisha lugha zetu.

Kwa hivyo, mimi naunga mkono Hoja hii na kumpongeza mheshimiwa Joyce Lay kwa kuileta wakati huu unaofaa. Ahsante sana.

**Hon. H.K. Njuguna:** Thank you so much, hon. Temporary Deputy Speaker. If Kiswahili was the major medium of instruction in this House, most of us would not be here. I have sat here listening to the contribution of Members. I realize that when you speak English, but without the Queen's accent, people laugh at you. This is even common amongst our children. However, when you are not able to communicate in Kiswahili, it is prestigious. We have gone through school and we know that English is the medium of instruction. It is high time we experienced a change of attitude. What is in a language? It carries the culture and traditions of the people. It is the pride of people. No wonder literary giants like Ngugi wa Thiong'o have chosen to communicate in Gikuyu in spite of being schooled in English to a point of being a Professor. When I speak in Gikuyu, I feel it and walk in it because therein lies the tradition of the Agikuyu. When you talk in Dholuo language, you are able to walk with the pride of the Luo. When you talk in English, there lies the customs and traditions of English. There is diversity in language. We accept today that Kiswahili is the linkage of all the 42 tribes in this country.

I support hon. Joyce Lay in her Motion. It is so fundamental. It should not be implemented tomorrow; it should have been implemented yesterday. I support it.

**Hon. Mustafa:** Ahsante sana Naibu Spika wa Muda kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia Hoja hii muhimu. Ningependa kuchukuwa fursa hii kumshukuru mheshimiwa Joyce Lay kwa kuileta Hoja hii katika Bunge. Kiswahili kinapendeza na kinafaa kutukuzwa ndipo kitumike katika nyanja muhimu kama vile sheria. Mimi nitakupa ninayoyajua katika sheria kuhusiana na Kiswahili. Niliwahi baada ya kushinda uchaguzi kupelekwa mahakamani na wapinzani wangu. Lugha iliyokuwa ikitumiwa ni Kiingereza. Wengi wa wafuasi wa wapinzani wangu walipofika mahakamani hawakuelewa kesi. Hii ni kwa sababu kila siku tulipokuwa tunatoka mahakamani wao wangerudi mitaani na kueneza mambo ambayo hayakuwa mahakamani kwa sababu walikuwa hawaelewi lugha ya Kiingereza. Kwa sababu hiyo naona umuhimu wa kutafsiri sheria zetu katika lugha ya Kiswahili.

Mimi naonelea kwamba ni muhimu tutenge angalau kikao kimoja kutoka katika vikao vinne ambavyo Bunge inavyo kila wiki ili kikao hicho kimoja kiendelezwe kwa lugha ya Kiswahili. Tukifanya hivyo basi tutasaidia kukuza Kiswahili. Aidha, kitendo hicho kitawashurutisha Wabunge kukienzi Kiswahili. Baadhi ya shule humu nchini zimetenga siku kadhaa kuwa siku za wanafunzi kuwasiliana kwa lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu wanafunzi hutahiniwa kwa lugha zote mbili; Kiingereza na Kiswahili. Ingekuwa vizuri pia sisi tuonyeshe mfano bora kama ilivyo katika mabunge mengine katika eneo la Afrika Mashariki na Kati.

Kwa hayo machache, ninaiunga mkono Hoja hii na kumpongeza tena Mhe. Lay pamoja na Mhe. Mbadi ambaye ameleta marekebisho ili Katiba iweze kutafsiriwa kwa Kiswahili.

**Hon. Sang:** Asante sana, Mhe. Naibu Spika wa Muda. Nimesimama kumuunga mkono dada yangu, Mhe. Joyce Lay. Tunafanana kidogo. Ninamshukuru sana kwa kuileta Hoja hii ambayo itatusaidia sisi wote. Kuna changamoto kila mahali kwa sababu watu wetu wanatumia Kiswahili kuongea. Tutapata changamoto nyingi tutakapotafsiri Kiingereza kwa Kiswahili. Tukitafsiri sheria zetu kwa Kiswahili, tutasaidika. Sijui kama



Mhe. Lay atanifunza Kiswahili kidogo. Hospitalini tuko na madaktari ambao wamesoma sana ambao wanaitwa *consultants*. Kwa Kiswahili, wanaitwa bingwa. Sijui wale madaktari ambao wanawatibu wamama wataitwa mabingwa wa nini.

Ninaunga mkono Hoja hii.

**Hon. Odanga:** Asante sana, Mhe. Naibu Spika wa Muda. Nami pia nataka kuiunga mkono Hoja hii ambayo imeletwa hapa na Mhe. Wanjala na kufanyiwa marekebisha na Mhe. John Mbadi. Naiunga mkono kwa sababu Kiswahili ni lugha yetu. Ni lugha ya Kiafrika na pia imetambuliwa katika Katiba kuwa lugha rasmi ya taifa. Ikiwa lugha rasmi, sioni urasmi wake sana isipokuwa katika Katiba.

Taasisi ya Mtaala katika Shule za Kenya imekitambua Kiswahili kuwa lugha ya lazima kwa wanafunzi katika shule za msingi na shule za upili. Hiyo inamaanisha kuwa Wakenya wengi sana wanakielewa Kiswahili. Inafaa kwamba stakabadhi zote rasmi zitafsiriwe kwa lugha ya Kiswahili ikiwemo Katiba ya Kenya.

Pia, Katiba inaelekeza kuwa Wakenya wote wana haki ya kupata habari. Ikiwa wana haki ya kupata habari, basi habari hiyo iwekwe katika lugha ambayo wanaelewa vizuri na wanaitumia katika maisha yao ya kila siku. Ikiwa hii ni lugha yetu, ni vizuri kuichangamkie zaidi kuliko lugha za kigeni kama vile Kiingereza ambayo ni lugha inayoendeleza ukoloni mambo leo. Ikiwa tunataka kujikomboa kutoka minyororo ya ukoloni, ni lazima tuienzi na kujivunia lugha yetu ya Kiswahili.

Kwa hayo machache, ninaunga mkono.

**Hon. (Ms.) Ombaka:** Thank you, hon. Temporary Deputy Speaker for this opportunity. I support this Motion. I acknowledge Mhe. Wanjalah for this wonderful Motion. Kenya is a multilingual society. We have 42 languages, but what unites us is one language that is Kiswahili.

Therefore, I believe that once this Constitution is translated into Kiswahili, we will be moving towards the unity of a nation. We are doing well in terms of Kiswahili being spread around so that Kenyans can speak it. Already, we have many books that are translated into Kiswahili. It is not only the Bible but dictionaries as well. We also have FM radio stations presenting their news in Kiswahili. We have *Julius Caesar*, one of the greatest books written by William Shakespeare, which was translated into Kiswahili by the late Julius Nyerere, the former President of Tanzania. That shows you the power of Kiswahili in this country. I, therefore, support this Motion.

Thank you very much.

## ADJOURNMENT

**The Temporary Deputy Speaker** (Hon. (Ms.) Shebesh): Hon. Members, the time being 1 p.m., this House stands adjourned until this afternoon at 2.30 p.m.

The House rose at 1.00 p.m.